

Kushiriki lazima kuegemee kwenye Aqidah na kuwiana na hukmu za Kiislamu. Upigaji kura katika mifumo inayotunga sheria kinyume na mwongozo wa Mwenyezi Mungu ni haramu, kwani inaidhinisha sheria zilizotungwa na mwanadamu juu ya sheria za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema,

[أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ]

“Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?” (Quran, Surah Al-Ma'idah, Ayah 50). Uchaguzi wa urais na bunge, ambapo wagombea huidhinisha sheria kinyume na Uislamu, wanalegeza msimamo kwa kanuni za Kiislamu, na kuunga mkono mfumo wa utawala usio wa Kiislamu. Mwenyezi Mungu anaonya,

[وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ]

“Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (Quran, Surah Al-Ma'idah, Ayah 44).

Njia bora zaidi kuelekea mbele inaakisi njia ya Mtume Muhammad (saw) na Maswahaba zake, ambao hawakulegeza msimamo kwa maadili ya Kiislamu kwa ajili ya mapato ya muda mfupi. Mwenyezi Mungu ameamuru,

[لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ]

“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.” (Quran, Surah Al-Ahzab, Ayah 21). Mwongozo huu unawataka Waislamu kuunda Kitambulisho cha kisiasa cha Kiislamu kinachowiana na kanuni za Mwenyezi Mungu.

Jamii ya Kiislamu ina majukumu muhimu, ndani na kimataifa. Ndani ya nchi, Waislamu wanapaswa kuunda majukwaa yao ya kisiasa, si kwa madhumuni ya kupiga kura, bali kuimarisha kitambulisho cha Kiislamu, kujenga mafungamano ya jamii, na kushiriki katika dawah. Kwa kushughulikia masuala ya kijamii kama vile ukosefu wa makao, mwanya wa kiuchumi, na maadili ya kifamilia, Waislamu wanaweza kuonyesha masuluhisho ya Uislamu kwa matatizo ya kijamii, wakiyawasilisha kama jibu kwa changamoto za kisasa. Uwepo imara wa Waislamu, katika jamii na kwenye mitandao ya kijamii, unaweza kushajiisha kutafakari juu ya hekima ya mafundisho ya Kiislamu.

Ulimwenguni kote, Umma wa Kiislamu lazima ushirikiane ili kuregesha umoja na mamlaka, kuondoa ufidadi, na kufukuza ushawishi wa kikoloni. Ruwaza hii inayoegemezwa katika mfumo wa Kiislamu, inalenga kuondosha tawala za kidhalimu na kusimamisha utawala wa uadilifu na huruma wa Uislamu kupitia Khilafah. Mtume (saw) alibashiri maregeo hayo, akasema: «**Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya utume.**» (Musnad Ahmad). Kusimamishwa tena kwa Khilafah kunaahidi kuhuisha uadilifu na amani, kutekeleza maneno ya Mwenyezi Mungu.

[وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ]

“Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.” (Quran, Surah 21:107).

Kwa kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu, Waislamu wamefaradhihwa kufanya kazi kuelekea ruwaza hii, wakiungana chini ya bendera ya Uislamu kuongoza jamii kwa huruma na uadilifu. Mwenyezi Mungu anakumbusha,

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ]

“Enyi mlio amini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele.” (Quran, Surah Al-Anfal, Ayah 24).

H. 22 Rabi' II 1446

M. : Ijumaa, 25 Oktoba 2024

Hizb-ut-Tahrir
Amerika